**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka: 2004**

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.

3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama **30** kila moja.

4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja sifa nne za mazingira bora ya ujifunzaji lugha darasani.

2. Eleza umuhimu wa mwalimu kutumia lugha sanifu na fasaha anapowafundisha watoto. (Sababu nne).

3. Bainisha matumizi manne ya vikaragosi (puppets) katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza.

4. Fafanua kwa kifupi jinsi mchezo wa "Tafuta Kitu Kilichofichwa" unavyoweza kukuza stadi ya kusikiliza na kufuata maelekezo.

5. Ainisha matatizo manne ya kimaumbile yanayoweza kuathiri uwezo wa mtoto wa kutamka maneno vizuri.

6. Kwa nini mwalimu anapaswa kufanya marudio ya mara kwa mara anapofundisha herufi au maneno mapya? Toa hoja nne.

7. Eleza kwa kifupi jinsi unavyoweza kutumia shughuli ya upishi rahisi (k.m. kutengeneza sharubati) kufundisha lugha. (Hoja nne).

8. (a) Eleza maana ya dhana "kushika kalamu kwa njia sahihi".

   (b) Taja shughuli mbili za kurekebisha mtoto anayeshika kalamu vibaya.

9. Bainisha changamoto nne za kutumia mbinu ya maswali na majibu katika darasa lenye watoto wengi.

10. Fafanua kwa kifupi jinsi kuimba tenzi na nyimbo za jadi kunavyochangia katika kuhifadhi na kukuza lugha ya Kiswahili kwa mtoto.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

11. "Ukosefu wa zana za kufundishia na kujifunzia ni kikwazo kikubwa katika ufundishaji wa stadi za lugha." Jadili kauli hii kwa kutoa hoja tano.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

12. Mtoto mmoja darasani kwako ana tatizo la kigugumizi. Chambua mikakati mitano utakayoitumia kumsaidia awapo darasani ili asijisikie mnyonge.

13. Fafanua umuhimu wa kutumia hadithi za picha katika kumjengea mtoto msingi wa kusoma na kupenda vitabu. (Hoja tano).

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

14. Eleza hatua tano utakazopitia ili kuandaa na kutumia zana ya "gurudumu la herufi" (letter wheel) kufundisha uhusiano kati ya herufi na sauti.

15. "Mwalimu mbunifu anaweza kugeuza hata takataka kuwa zana bora ya kufundishia." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano mitano ya zana unazoweza kutengeneza kwa kutumia malighafi zilizotumika (k.m. chupa za plastiki, makatoni).

16. Chambua faida tano za mwalimu kutumia mbinu ya uchunguzi kama njia ya kupima maendeleo ya lugha ya mtoto.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org